TANGAZO LA SERIKALI Na. 53 la tarehe 26/1/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWAKATIKA ENEO LA SIMAMBWE YA MWAKA 2024

Jina

**1.** Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Simambwe ya mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

**2.** Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

**3.** Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G1 yenye majira-nukta 568303MS, 9007707KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G2 yenye majira-nukta 568831MS, 9007027KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G3 yenye majira-nukta 568448MS, 9006715KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G4 yenye majira-nukta 56346MS, 9005998KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G5 yenye majira-nukta 568069MS, 9006097KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G6 yenye majira-nukta 568260MS, 9006442KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G7 yenye majira-nukta 567982MS, 9006805KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 535 yenye majira-nukta 568051MS, 9006972KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.8 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*